

RIPOTI FUPI JUU YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA “KUKUZA USHIRIKI WA ASASI ZA KIRAIA KATIKA MIDAHALO YA KISERA NA MAENDELEO KATIKA NGAZI ZOTE – TAREHE 29 JANUARI, 2019

1. Utangulizi

Ndugu waandishi wa Habari

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuruni nyote kwa kuhudhuria katika mkutano wetu huu mfupi wa kupokea ripoti ya utekelezaji wa mradi wa kukuza ushiriki wa asasi za kiraia katika midahalo ya sera na maendeleo chini ya programu ya Kusaidia asasi za kiraia Zanzibar (ZANSASP) inayofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya (EU).

ZANSASP ni programu ya pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Umoja wa Ulaya. Programu hii ni ya miaka 3 kuanzia mwaka 2015 na inatekeleza kaitka wily azote za Unguja na Pemba.

2. Mradi unaotekelezwa na ANGOZA

Ndugu waandishi wa habari

ANGOZA ni miongoni mwa asasi zilizofanikiwa kupata ufadhili wa kutekeleza mradi wa kukuza ushiriki wa asasi za kiraia katika majadiliano ya sera na maendeleo Zanzibar kupitia programu ya ZANSASP. Mradi huo umepangwa kutekelezwa katika kipindi cha miezi 11 kuanzia Juni 2018 mpaka April 2019

2.1 Shughuli kuu za mradi kama ifuatavyo:

- (i) Kufuatilia uundwaji wa kitengo cha uratibu wa asasi za kiraia katika Wizara husika
- (ii) Kusaidia wajasiriamali katika kupata soko la bidhaa zao kupitia mawasiliano ya mtandao
- (iii) Kukuza uelewa wa wananchi juu ya nishati mbadala (Renewable Energy)
- (iv) Kukusanya maoni ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali juu ya uanzishwaji wa Baraza la mashirika yasiyo ya Kiserikali
- (v) Kuandaa KONGAMANO la mwaka la asasi za kiraia kwa mwaka wa 2019

2.2 Utekelezaji wa shughuli za mradi

2.2.1 Uundwaji wa kitengo cha uratibu (Baraza la asasi zisizo za kiserikali)

Utekelezaji wa shughuli hii haukuweza kufanyika kutokana na kuondoshwa kwa shughuli za asasi za kiraia kutoka katika Ofisi ya Rais Katiba na Sheria, Utawala wa Umma na Utawala Bora na kuhamishiwa katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

2.2.2 Kusaidia wajasiriamali katika kupata soko la bidhaa zao kupitia mawasiliano ya mtandao

Mafunzo juu ya Habari, mawasiliano na Teknolojia (ICT) yameendeshwa kwa wajasiriamali wa Unguja na Pemba na mwisho wa mafunzo mtaalamu wa ICT aliyopo ANGOZA aliweza kufungua ukurasa maalum unaojulikana kama soko la wazi “Open Source Market” ambao unaunganisha baina ya muuzaji na mnunuaji na kutangaza biashara hizo kupitia mitandao.

2.2.3 Kukuza uelewa wa wananchi juu ya nishati mbadala (Renewable Energy)

ANGOZA iliendesha mafunzo kwa wadau mbali mbali wanaoishi katika jamii juu ya matumizi ya nishati mbadala na ufanisi. Mafunzo hayo yaliendeshwa Unguja na Pemba kwa dhamira ya kukuza uelewa na hatimae kushajiika ili kuweza kutumia nishati mbadala na kutumia umeme kwa ufanisi.

2.2.4 Kukusanya maoni ya asasi za kiraia juu ya uanzishwaji wa baraza la Mashirikia yasiyo ya kiserikali (NGOs)

ANGOZA tayari imekusanya maoni ya wadau mbalimbali kutoka Pemba na Unguja juu ya uanzishwaji wa baraza la NGOs kupitia mikutano na wadau wa asasi zisizo za kiserikali katika maeneo ya Unguja na Pemba, na hatimae kuweza kutayarisha waraka juu ya mapendekezo hayo.

Hivyo hatua iliyobaki ni kuwasilisha mapendekezo hayo Serikalini kwa kukamilisha mchakato wa uundwaji wa baraza hilo.

2.2.5 Kuandaa KONGAMANO la asasi za kiraia kwa mwaka 2019

Kuandaa KONGAMANO la mwaka la asasi za kiraia kwa mwaka 2019 ni miongoni mwa shughuli kuu ambayo inahitaji maandalizi ya muda mrefu, katika kufanikisha shughuli hii, Kamati ya maandalizi iliweza kuundwa na ina wajumbe saba wawili wanatoka Serikalini na watano wanantoka asasi za kiraia. Jumla ya mikutano minne ya kamati tayari imeshafanyika na mkutano wa tano unatarajia kufanyika tarehe 14 au 15 ya mwezi wa Febuari 2018. Kwa ujumla maandalizi yanakwenda vizuri. Kongamano la mwaka 2019 limepangwa kufanyika tarehe 26 na 27 Febuary 2019, na litakuwa na kauli mbiu isemayo ***“Asasi za kiraia kwa maendeleo endelevu”***.

3.0 HITIMISHO

Ndugu waandishi wa habari

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mradi huu wa kukuza ushiriki wa asasi za kiraia katika sera na maendeleo chini ya programu ya ZANSASP ni kama upatikanaji wa maoni ya uundaji wa baraza kutoka kwa wadau mbali mbali wa Asasi zisizo za kiserikali, kuwepo kwa muamko katika jamii juu ya matumizi ya nishati mbadala, kuwepo kwa wajasiriamali ambao wanaweza kujitangaza na kuuza biashara zao kwa kupitia mtandao

Aidha changamoto zilizopatikana katika kufanikisha maazimio hayo ni uwepo kwa idadi ndogo ya wajasiriamali walioweza kuuza na kutangaza biashara zao kwa kutumia mtandao kutokana na kutokuwa na vifaa vya tehamu na bidhaa zenye ubora. Kuchelewa kufanyika kwa mrekebisho ya sheria inayohusiana na shughuli za asasi za kiraia na kupelekea kuchelewa kuazishwa kwa kitengo cha uratibu wa shughuli za asasi za kiraia katika Wizara mpya iliyohamishiwa shughuli za asasi za kiraia. ANGOZA inaendelea kuwasiliana na Wizara husika ili kuondoa changamoto hizo

Ahsanteni kwa kunisikiliza